MAJUKUMU YA KISHERIA YA IDARA YA UTUMISHI WA WALIMU.

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

1.0 Utangulizi

Katika kipindi cha wiki nne zijazo tutachapisha makala juu ya majukumu ya Idara ya Utumishi wa Walimu, Usajili wa walimu, Kuthibitishwa kazini kwa Walimu na Kubadilisha Cheo au kazi katika utumishi wa Walimu ili kutoa ufafanuzi juu ya maswali tuliyoandikiwa au kupigiwa simu na wasomaji wetu wakitaka kuelewa juu ya masuala hayo. Kwa wiki hii tutachapisha juu ya majukumu ya Idara ya utumishi wa walimu. Idara ya Utumishi wa Walimu ni miongoni mwa Idara za 4 za Tume ya Utumishi wa Umma iliyoundwa chini ya Kifungu cha 15 cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya 2002. Lengo la kuchapisha makala haya ni kwaelimisha wadau wa Idara ili waweze kufahamu majukumu ya Idara yao na kupata fursa ya kuwajibika vizuri zaidi na kuijengea Idara uwezo wa kutekeleza kwa mafanikio majukumu yake.

2.0 Majukumu ya Idara ya Utumishi wa Walimu

Idara ya Utumishi wa Walimu tofauti na Idara nyingine za Tume imepewa Mamlaka ya kushughulikia Ajira na Nidhamu ya Walimu. Mamlaka hayo ya Kisheria yamebainishwa kwenye Kifungu cha 6(4) cha Sheria Na. 8 ya 2002 ambapo Idara hushughulikia ajira, usaili, kuthibitisha Walimu, kupandisha Vyeo na masuala ya Nidhamu.

2.1 Ajira

Idara ya Utumishi wa Walimu ndiyo inayoshughulikia ajira zote za Walimu katika Utumishi wa Umma. Ifahamike kuwa TSD siyo mwajiri wa walimu bali ni Mamlaka ya Ajira ikimaanisha Idara ndiyo inayotawala na kusimamia ajira rasmi katika Utumishi wa Walimu.

2.2 Usaili

Idara hupokea mikataba na kuisajili ambapo walimu hupewa nambari zao za usajili katika ualimu.

2.3 Kupandisha vyeo walimu

Idara ndiyo mamlaka ya kuwapandisha walimu vyeo waliotimiza sifa zinazohitajika. Waajiri watawasilisha mapendekezo yao kwa Idara ambayo kwa kutumia sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo itawapandisha vyeo walimu husika.

3.0 Mamlaka ya Nidhamu.

Idara ya Utumishi wa Walimu ndiyo Mamlaka ya Nidhamu kwa Walimu katika utumishi wa Umma.

Idara hii tofauti na Idara nyingine za Tume, imepewa uwezo wa kushughulikia masuala ya Nidhamu ya walimu. Idara inazo Kamati za wilaya na Mkoa ambazo kwa mujibu wa Kanuni Na. 121 ya Kanuni za Utumishi wa Umma 2003, zimepewa uwezo wa kusikiliza mashauri ya Nidhamu ya Walimu na kutoa adhabu mbalimbali ukiondoa ya kufukuzwa kazi ambayo hutolewa na Makao Makuu ya Idara.

4.0 Majukumu mengne ya Idara

Idara inayo majukumu mengine inayoyatekeleza katika kuwahudumia walimu.

- **Pensheni na Mirathi:**

  Idara inashughulikia ukokotoaji wa malipo ya mirathi na pensheni.

- **Utafiti**:

Idara huendesha tafiti mbalimbali kuhusiana na Utumishi wa Walimu kwa lengo la kubaini kero na matatizo yanayoukabili utumishi wa walimu na kuishauri Serikali namna bora ya kuendesha utumishi huo nchini.

Kwa msingi huo majukumu ya Idara yameainishwa vizuri na sheria na yatatekelezwa kwa kuzingatia sheria, Kanuni na Taratibu.

5.0 Nini maana ya Idara kama Mamlaka ya Ajira na Nidhamu.

Kifungu cha 6(4) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya 2002 kimeipa Idara ya Utumishi wa Walimu uwezo wa kuwa Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu.

Kuwa Mamlaka ya Ajira na Nidhamu maana yake ni kuwa chombo cha kushughulikia masuala yote yahusuyo Ajira za Walimu na Nidhamu. Kwa maana hiyo, TSD ndiyo iliyopewa jukumu la ajira zote za Walimu katika Utumishi wa Umma ikiwa ni pamoja na Usajili kazini na kuwapandisha vyeo.

Kuhusu nidhamu, Idara ndiyo iliyopewa uwezo wa kusimamia na kudhibiti Nidhamu na Maadili ya Ualimu. Katika utekelezaji wa jukumu hilo Idara hufungua mashtaka dhidi ya mwalimu anayetuhumiwa kwa kosa la kinidhamu, kumsimamisha kazi na kumpa adhabu pale makosa yake yanapothibitika. Kwa ujumla jukumu la kuhakikisha kuwa walimu wanazingatia maadili ya kazi yao na kuchukua hatua kwa wasiozingatia ni la TSD.

Katika kutekeleza majukumu yake kama Mamlaka ya Ajira na Nidhamu, Idara ya Utumishi wa Walimu licha ya kuwa ni Idara ya Tume, haifanyi hayo kwa niaba ya Tume. Kwa msingi huo mwalimu ambaye hakuridhika na uamuzi wa Idara kuhusiana na shauri lake

anaweza kukata rufaa kwa Tume ambapo maamuzi ya Idara yatajadiliwa na kutolewa uamuzi kama Mamlaka nyingine ya Nidhamu iliyo nje ya Tume. Hivyo basi Tume haina ushawishi kwa Idara inapotekeleza majukumu yake na wala Idara haina ushawishi kwa Tume na inaposikiliza rufaa zilizokatwa dhidi yake.

5.0 Hitimisho

Idara ya Utumishi wa Walimu inawaomba wadau wote kuwa na ushirikiano wa karibu zaidi katika kutekeleza majukumu ya Idara kwani kwa kufanya hivyo hapo ndipo Idara itaweza kuboresha utumishi wa walimu na Elimu nchini.

Kama una maoni tafadhali tuandikie
Katibu,
Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma
S.L.P 9143
DSM

UMUHIMU WA KUSAJILI WALIMU

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

1.0 Utangulizi

Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 na 1995 kifungu 44(1) na (2), mwalimu ni yule aliyehudhuria na kufaulu mafunzo ya ualimu katika chuo kinachotambulika na Serikali. Mwalimu aliyehitimu na kufaulu mafunzo ya ualimu anatakiwa kupata cheti na kusajiliwa.

2.0 Usajili

Hatua ya kusajiliwa huanza wakati mwalimu anapopangiwa kituo cha kazi na mwajiri wake. Kwa walimu wa shule za msingi waajiri wao ni Wakurugenzi Watendaji wa Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya. Kwa Walimu wa shule za Sekondari na Vyuo waajiri wao ni Makatibu Wakuu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Elimu ya juu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mara baada ya kupangiwa kituo cha kazi mwalimu analazimika kujaza fomu za Mkataba wa Ajira na Mwajiri wake. Fomu hizo zinapatikana katika Ofisi za Tume ya Utumishi wa Umma, Idara ya Utumishi wa Walimu Wilayani. Ili kuweza kukamilisha kazi hii ni vyema mwalimu akawasiliana na Katibu wa Tume Wilayani ili aweze kupata maelekezo ya jinsi ya kujaza fomu hizo.